# Baada ya Kosa la Ushambuliaji, CalVCB Inaweza Kusaidia Kulipa Bili Zako

**TUNASAIDIA WAATHIRIWA WA:**

- Kushambuliwa
- Dhuluma kwa watoto
- Dhuluma za nyumbani
- Kuendesha gari ukiwa mlevi
- Dhuluma kwa wazee
- Makosa ya chuki
- Mauaji
- Ulanguzi wa binadamu
- Wizi wa kimabavu
- Dhuluma za kingono
- Unyemeleaji
- *... na makosa mengine*

**TUNAWEZA KUSAIDIA KULIPIA:**

- Ushauri
- Gharama za mazishi na maziko
- Kupoteza mapato
- Matibabu na huduma za meno
- Uhamisho
- Usalama wa nyumbani
- *... na gharama nyingine*

**victims.ca.gov**
**P.O. Box 3036**
**Sacramento, CA 95812**

**Viziwi na wenye shida ya kusikia: Piga Simu kwa California Relay Service kwa nambari 711*

## CalVCB husaidiaje?

- Waathiriwa wanaopata jeraha la mwili au jeraha la kihisia kutokana na vitisho vya kudhuriwa kimwili wanaweza kutimiza masharti ya kupokea msaada.
- CalVCB husaidia waathiriwa kulipa gharama zinazohusiana na kosa ambazo hazilipwi na chanzo kingine chochote.
- Baada ya ombi kukubaliwa, waathiriwa wanatimiza masharti ya kupokea msaada wa hadi $70,000. Baadhi ya vikomo vya msaada vinaweza kutumika.

## Nani anayetimiza masharti?

CalVCB inaweza kusaidia waathiriwa na familia zao kosa linapofanya California, au linapomfanyikia mkazi wa California katika jimbo au nchi nyingine. Uraia wa Marekani hauhitajiki ili kuomba msaada.

Waathiriwa wanaweza kutuma maombi ndani ya miaka saba baada ya kosa kufanyika, au baada ya miaka saba baada ya mwathiriwa kujua au kutambua kwamba jeraha au kifo kilitokea kwa sababu ya kosa. Waathiriwa wenye umri wa miaka 21 au chini yake wana hadi watakapofikisha umri wa 28 kutuma ombi.

## Ninatumaje ombi?

**TUMBA OMBI MTANDAONI** katika **victims.ca.gov**

Mtetezi **wa mwathiriwa** anaweza kukusaidia kutuma ombi. Nenda kwenye **victims.ca.gov/get-help** na uweke nchi yako.






*05/2026 [SWA]*